# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.10 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) DESEMBA 2021

# TSC YAENDESHA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA KADA SAIDIZI



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa hotuba ya kufungua mafunzo ya Watumishi wa Kada Saidizi wa TSC Novemba 8, 2021 jijini Dodoma.*

**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

## HONGERENI WALIMU KWA KAZI KUBWA MNAYOIFANYA

Tunawapongeza walimu kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuwalea watoto kimwili, kiroho, kiakili na kijamii ili waweze kuwa raia wema wa badae wanaoweza kuleta maendeleo chanya katika Nchi yetu.

Matokeo ya juhudi za walimu zinaendelea kuonekana kutokana na viwango vya ufaulu kuendelea kuongezeka kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Kuanzia mwezi Oktoba hadi mwishoni mwa mwezi Novemba, wanafunzi wa Darasa la Nne, Darasa la Saba, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne wamekuwa kwenye mitihani ya kitaifa ambapo walikuwa wanapimwa kwa namna walimu walivyowaandaa.

Tunapoelekea mwishoni mwa mwaka, ni imani yetu kuwa kila mwalimu ametimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kufundisha vipindi vyote alivyopangiwa kwa mujibu wa taratibu.

TSC tunawatakia walimu kila lililojema wakati wanapowaandaa wanafunzi kufanya mitihani yao ya kumaliza muhula wa pili wa masomo. Tutaendelea kufanya kazi kwa karibu na walimu, kupokea kero na malalmiko yao na kuyatafutia ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, tutaendelea kuhakikisha walimu wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Miiko na Maadili ya kazi hiyo ili tuendelee kuandaa wanafunzi bora kwa ustawi wa Taifa letu.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# TSC YAENDESHA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA KADA SAIDIZI



*Baadhi ya watumishi wa Kada Saidizi wakisikiliza hotuba ya ufunguzi wa mafunzo yao kutoka kwa Mwenyekiti wa TSC, Prof. Lazaro Komba (hayupo pichani) Novemba 8, 2021 jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imewataka Kaimu Katibu Wasaidizi 139 Wilayani wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kuacha kuwabambikizia makosa walimu ili wasionekanane watendaji wazuri jambo linalosababisha kutopandishwa kwao madaraja.

Aidha imepiga marufuku kuomba au kuweka mazingira ya rushwa kwa walimu ili waweze kuwapendekeza majina yao katika upandishwaji madaraja.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. David Silinde, wakati kifungua Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume kutoka wilaya 139 kilichofanyika jijini Dodoma.

Mheshimiwa Silinde alisema hataki kusikia walimu wanabambikiwa makosa na Makatibu hao na endapo atabaini hilo hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

"Sitaki kusikia suala la kumbambikizia makosa walimu. Hiyo inachangia kumkosesha mwalimu nafasi ya kupandishwa daraja,"alisema Silinde.

Hata hivyo alisema hakuna sababu ya kuweka bifu na walimu na kusababisha kuwabambikizia makosa jambo ambalo wanajenga uadui baina yao na kushusha morali ya utendaji kazi katika maeneo yao.

Mbali na hilo alisema anapiga vita suala la rushwa wanalodaiwa walimu ili waweze kupandishwa daraja katika ngazi walizokuwa nazo shuleni kwani Katibu Wasaidizi wanatakiwa kutenda haki na sio kuingia katika ubadhirifu, uvunjaji Sheria, na uonevu.

Alisema TAMISEMI ikibaini kuna Katibu Msaidizi anayefanya hivyo basi hatua kali zitachukuliwa dhidi yake kwani Serikali inawaamini sana kutokana na utendaji kazi wao.

"Nawapongeza sana kwenye



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (mwenye suti nyekudu kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa mafunzo ya watumishi wa Kada Saizi. Kushoto kwa Mwenyekiti ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na wa kwanza upande wa kulia wa Mwenyekiti (kwa Waliokaa) ni Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama. Wengine (waliokaa) ni wakufunzi wa Mafunzo hayo.*

suala la kupandisha walimu madaraja, lakini nasisitiza kuwa rushwa iachwe kwani walimu wenye sifa wanapaswa kupewa nafasi ya kupandishwa madaraja,"alisema Silinde.

Alisema rushwa ni adui wa haki na haipaswi kuingizwa kazini hivyo ni vema wakaliacha na kuwapa nafasi walimu ya kufanya kazi kwa bidi bila makandokando yoyote.

Akizungumzia suala la fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais alisema jumla ya shilingi billioni 536.6 ambazo zilitolewa TAMISEMI na shilingi billioni 304 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya elimu hivyo kusisitiza ziende zikatumike ipasavyo katika miradi hiyo.

Mbali na hilo alizitaka halmashauri kuhakikisha zinawapatia mara moja Kaimu Katibu Wasaidizi Wilaya ofisi zenye hadhi ya kufanyia kazi na sio kuwaacha wakifanya kazi katika mazingira ambayo hayastahili na atakayekwenda kinyume na maelekezo hayo Wizara itachukua hatua kwa namna ambavyo itaona inafaa.

Ukiacha hilo alisema ofisi yake inaliangalia suala la bajeti kwa jicho la pekee ili kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira yenye weledi ambayo yataifanya Tume na walimu kwa ujumla wao kufanya kazi kwa weledi mkubwa na kuleta mafanikio tarajiwa nchini.

Silinde alitoa wito kwa walimu kushiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu hapa nchini.

Kwa upande wake Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama, alisema Tume hiyo itahakikisha fedha zilizotolewa zitatumika ipaswavyo katika miradi ambayo inatekelezwa hapa nchini.

Alisema wanaihakikishia OR-TAMISEMI kila kitu kilichopangwa kitakwenda ipasavyo ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati.

"Tumejipanga kuhakikisha tunatekeleza kile tulichoagizwa hivyo msiwe na wasiwasi na Tume," alisema Nkwama.

Naye Mwenyekiti wa TSC Profesa Willy Komba alisema vitendo vya uonevu havitakuwa na nafasi katika Tume hiyo, hivyo watahakikisha kila mmoja anafanya kazi yake bila ya kuonewa na mtu.

Alisema Tume hiyo inasimamia haki hivyo suala la rushwa halipewi nafasi kwenye utendaji wa Tume wa kila siku.

# TSC YAENDESHA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA KADA SAIDIZI



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (mwenye suti nyekudu kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa mafunzo ya watumishi wa Kada Saizi. Kushoto kwa Mwenyekiti ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na wa kwanza upande wa kulia wa Mwenyekiti (kwa Waliokaa) ni Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama. Wengine (waliokaa) ni wakufunzi wa Mafunzo hayo.*

# TSC TANGA YAING'ARISHA HALMASHAURI YA JIJI, UPANDISHAJI VYEO WATUMISHI WA UMMA



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanga, Naima Twalib akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami wakati walipofanya mazungumzo yaliyolenga kujua utekelezaji wa majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo.*

**Na. Mwandishi Wetu, Tanga**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Tanga imefanya vizuri katika zoezi la upandishaji madaraja walimu lililofanyika mwaka huu 2021 na kuifanya Halmashauri ya Jiji la Tanga kushika nafasi ya kwanza kitaifa katika halmashauri zilizofanya vizuri katika zoezi la kupandisha madaraja watumishi wa Umma.

Hayo yalibainishwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Tanga, Naima Twalib wakati wa mahojiano na jarida hili yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC wilayani hapo ambapo alisema Halmashauri hiyo ilipatiwa cheti cha kutambua kazi hiyo kilichotolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Juni 22, 2021.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alieleza kuwa mafanikio hayo yametokana na ushirikiano uliopo kati ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji hususan Maafisa Elimu, Maafisa Utumishi na TSC kitu ambacho kimefanya shughuli hiyo kwenda kwa haraka na kumalizika kwa wakati.

"Hapa tuna ushirikiano mzuri sana, hata katika zoezi la kupandisha madaraja walimu hatukupata ugumu kwa kuwa hatukuwa na mivutano hata kidogo. Matokeo ya ushirikiano huu ndiyo yalifanya Halmashauri kushika nafasi ya kwanza katika Halmashauri zote kwa kufanya vizuri kwenye zoezi hilo, na kama unavyojua sehemu kubwa ya watumishi wa umma ni walimu," alisema.

Alifafanua kuwa katika zoezi hilo jumla ya walimu 1013 walipandishwa vyeo ambapo katika idadi hiyo walimu 546 ni wa Shule za Msingi na walimu 467 ni wa Shule za Sekondari huku walimu 70 wa shule za msingi na walimu 87 wa shule za sekondari walibadilishiwa vyeo/kazi.

Aliongeza kuwa idadi hiyo ya walimu waliopandishwa vyeo ndio waliostahili kupanda huku akisisitiza kuwa hakuna aliyekuwa na sifa za kupanda ambaye hakupandishwa kwa sababu yoyote ile.

Vilevile, alieleza kuwa taratibu za kuhakikisha walimu waliopandishwa madaraja wanapata mishahara yao mipya zilifanyika kwa wakati na wahusika wote walibadilishiwa mishahara yao mapema kitu ambacho kimeondoa malalamiko yaliyokuwepo siku za nyuma kutokana na mishahara kutobadilika kwa wakati.

"Miaka ya nyuma tulizoea mwalimu anapandishwa daraja leo lakini inachukua muda mrefu kupata mshahara wa cheo kipya. Hili limechangia walimu kuwa na madeni ya muda mrefu wanayoidai serikali na kusababisha malalamiko mengi. Lakini kwa awamu hii tunashukuru kila kitu kilikwenda vizuri na kila aliyepanda tayari

# TSC TANGA YAING'ARISHA HALMASHAURI YA JIJI, UPANDISHAJI VYEO WATUMISHI WA UMMA



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Tanga.*

ana mshahara wa cheo chake,". Alisema Naima

Aliongeza kuwa pamoja na ushirikiano uliokuwepo kati ya mwajiri na TSC, zoezi hilo lilifanyika kwa ufanisi kutokana na kuwepo kwa vitendea kazi vya kutosha ikiwemo kompyuta, printer na shajala ambavyo vimekuwa vikitolewa na Tume Makao Makuu kwenye ofisi za Wilaya.

Wilaya hiyo ina jumla ya walimu 2183 ambapo kati ya hao walimu 1284 wa shule za msingi na walimu 899 ni wa shule za sekondari huku kukiwa na jumla ya shule za msingi 80 na sekondari 26 ambazo walimu wake wanahudumiwa na TSC kwa mujibu wa sheria.

Kiongozi huyo anaendelea kwa kueleza kuwa hali ya nidhamu ni nzuri kutokana na elimu inayotolewa mara kwa mara juu ya sheria kanuni na taratibu zinazoongoza kada ya hiyo ambapo walimu wengi wamekuwa wanazingatia taratibu husika.

Licha ya mafanikio likuki yaliyopatikana katika ofisi hiyo, kiongozi huyo alieleza kuwa kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika ni moja ya changamoto zinazokwamisha utoaji huduma bora kwa wakati hususan pale ofisi yake inapohitaji kutembelea walimu katika maeneo yao ya kazi.

Hivyo, alimuomba Katibu wa TSC kuona namna anavyoweza kuisaidia ofisi hiyo katika suala la usafiri ili iweze kuendelea kutoa huduma kwa walimu katika ubora unohitajika.



Certificate of Appreciation

presented to

Tanga City Council

CATEGORY: Public Institutions - Local Government Authorities

WINNER No. 1

In recognition of Outstanding Performance in

Administration and Human Resource Management in the Public Service

Conferred in Dodoma on the 22nd day of June, 2021 during AHRM Annual Conference

Dr. Laurean J. P. Ndumbaro
PERMANENT SECRETARY
PRESIDENT'S OFFICE, PUBLIC SERVICE MANAGEMENT AND GOOD GOVERNANCE

*Cheti cha pongezi kilichotolewa kwa Halmashauri ya Jiji Tanga.*

# NKWAMA AWATAKA WATUMISHI TSC KUFANYA KAZI KWA WELEDI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea na watumishi wa Kada Saidizi (hawapo pichani) wakati wa mafunzo ya watumishi hao yaliyofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amewataka watumishi wa Tume hiyo kufanya kazi kwa bidii, weledi na maadili ili kuiwezesha ofisi hiyo kufikia malengo yake katika kutoa huduma bora kwa wateja.

Nkwama alitoa kauli hiyo wakati wa mafunzo ya watumishi wa TSC wa kada saidizi yaliyofanyika hivi karibuni jijini Dodoma na kuhusisha watumishi wa kada za Makatibu Muhtasi, Watunza Kumbukumbu pamoja Wasaidizi wa Ofisi.

Alieleza kuwa kumekuwa na changamoto mbalimbali katika utendaji kazi kwa baadhi ya watumishi kitu kinachosababisha kinarudisha nyuma jitihada za tume hiyo kufikia malengo yake hivyo, Menejimenti ya TSC iliona kuna haja ya kutoa mafunzo hayo ili kutatua changamoto hizo.

"Katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku tumegundua changamoto zilizopo kwa baadhi ya watumishi ndiyo maana tunaendelea kutoa mafunzo ili kuwajengea uwezo muweze kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Maadili ya kazi katika maeneo yenu," alisema Nkwama.

Nkwama alitaja suala la baadhi ya watumishi kutokuwa waadilifu katika kutunza siri za ofisi kuwa ni moja ya changamoto zilizoonekana katika utendaji wa siku kwa siku kwa baadhi ya watumishi huku akisistiza kuwa moja ya maadili ya mtumishi wa umma ni kutunza siri na kuweka wazi kuwa mtumishi anayekwenda kinyume na utaratibu huo hawezi kuvumiliwa.



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (kushoto) akiwa na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati wa mafunzo ya watumishi wa Kada Saidizi yaliyofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.*

# NKWAMA AWATAKA WATUMISHI TSC KUFANYA KAZI KWA WELEDI



*Baadhi ya watumishi wa Kada Saidizi wakiwa katika ukumbi wa mafunzo.*

Changamoto nyingine iliyobainishwa na kiongozi huyo ni baadhi ya watumishi wanauhusika katika kupokea na kusambaza barua kutoziwasilisha sehemu zinapotakiwa kufika kwa wakati kitu ambacho kinaathiri Tume hiyo kwa ujumla.

"Tumegundua wapo baadhi yenu ambao wanatoa siri za ofisi kitu ambacho wote mnajua kuwa ni kinyume na taratibu za kazi. Baadhi yenu mnaletewa barua lakini hamzigongi mhuri kwa wakati, mwisho tunakuja kumwambia mteja ulileta barua yako nje ya muda wakati sio kweli. Barua zingine zinatakiwa zisambazwe kwa wahusika na ni za haraka lakini unakuta zinakaa siku mbili hazijasambazwa, hiyo sio sawa na siwezi kuwavumilia watu wenye tabia hizi," alisema Nkwama.

Katibu huyo aliendelea kueleza kuwa baadhi ya watumishi wanaohusika na uchapaji wa barua hawatekelezi wajibu wao inavyotakiwa kutokana na kutozingatia taratibu na miongozo ya uandishi wa nyaraka hizo hivyo mafunzo hayo yatasaidia kuwakumbusha namna ya kutekeleza majukumu hayo.

Katibu huyo alieleza TSC imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa watumishi wake wa kada zote ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya ofisi hiyo.



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa RasilimaliWatu, Moses Chitama akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya watumishi wa Kada Saidizi yaliyofanyika hivi karibuni Jijini Dodoma.*




*Mmoja wa Wawezeshaji wa Mafunzo ya Watumishi wa Kada Saizi, Dkt. Hamisi Amani kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma akiwasilisha mada wakati wa mafuzo hayo.*

# TSC NEWALA YAHAMASISHA WANAFUNZI KUJIEPUSHA NA UHUSIANO WA KIMAPENZI

**Na. Mwandishi Wetu, Newala**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Newala imefanya kongamano la mafunzo kwa wanafunzi wa kike wa Shule ya Msingi Kitangiri Mazoezi na Shule ya Sekondari Maputi zilizopo wilayani hapo kwa lengo la kuwahamasisha wanafunzi wa kike kujiepusha na uhusianao wa kimapenzi.

Kongamano hilo lililofanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa Chuo cha Walimu Kitangiri lilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Newala, Alhaji Rajabu Kundya ambaye aliwataka wanafunzi wa kike kuhakikisha wanazingatia masomo yao na kuachana na tabia ya kijiingiza katika mapenzi ili waweze kufikia ndoto zao.

Kundya aliewaeleza wanafunzi hao kuwa wanategemewa na wazazi, jamii na taifa hivyo wanapaswa kuwa na nidhamu na bidii katika masomo na kuepuka kila aina ya vishawishi ambavyo vitasababisha kuharibu mipango yao ya baade hususan katika elimu.

Naye Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Newala, Asha Chambanda alisema kuwa wapo baadhi ya walezi na waliimu wasio waadilifu ambao huwarubuni watoto wa kike kwa lengo la kufanya nao mapenzi kitu ambacho kinarudisha nyuma maendelmeo ya watoto hao na Taifa kwa ujumla.

Hivyo, wamewasihi wale wote wenye tabia hiyo kuacha mara moja ili wanafunzi hao waweze kupata haki yao ya kupata elimu katika mazingira salama na waweze kuwa na mchango chanya kwa jamii na taifa hapo baadae.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Newala, Asha Chambanda akiongea katika kongamano la mafunzo kwa wanafunzi wa kike lililofanyika hivi karibuni wilani Newala, kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya hiyo Alhaji Rajabu Kundya.*



*Mkuu wa Wilaya ya Newala, Alhaji Rajabu Kundya (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na wadau mbalimbali wa elimu waliohudhuria kongamano la mafunzo kwa wanafunzi wa kike lililofanyika hivi karibuni wilani Newala.*





*Wanafunzi wakiwa kwenye kongamano la mafunzo kwa wanafunzi wa kike lililofanyika hivi karibuni wilani Newala.*

# TSC KIBAHA YAPIGA HATUA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibaha, Marco Bahebe akimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa mahojiano maalum yaliyofanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Kibaha.*

**Na. Mwandishi Wetu, Kibaha**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibaha huenda ikawa miongoni mwa Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya zinazofanya vizuri zaidi katika kusimamia masuala ya nidhamu na Maadili kwa walimu.

Hilo limebainika hivi karibuni wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipotembelea ofisi hiyo na kufanya mahojiano maalumu na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya hiyo, Marco Bahebe kwa lengo la kufahamu mandeleo ya Wilaya hiyo katika kusimamia utumishi wa walimu.

TSC Wilaya ya Kibaha inasimamia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji Kibaha na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha a,napo Halmashauri ya Mji Kibaha ina jumla ya Walimu 1531 wanaofundisha shule 42 za msingi na walimu 676 wanaofundisha shule 12 za sekondari, hivyo kufanya halmashauri hiyo kuwa na jumla ya walimu 1531 na shule 54 za serikali ukiachilia mbali shule zinazosimamiwa na Shirika la Elimu Kibaha.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kuna jumla ya walimu 519 ambao wanafundisha shule za msingi 39 huku walimu wa sekondari wakiwa ni 317 wanaofundisha shule 8, na hivyo kufanya Hamlashauri hiyo kuwa



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibaha, Marco Bahebe (kulia) akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami wakati wa ziara ya kiongozi huyo wilayani Kibaha hivi karibuni.*

# TSC KIBAHA YAPIGA HATUA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU

na jumla ya walimu 836 na shule 47.

Bahebe alieleza kuwa licha ya Wilaya hiyo kuwa na jumla ya walimu 2,367, katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Novemba 2021 hakuna shauri la nidhamu hata moja lililoripotiwa kwa ngazi ya shule wala ngazi ya Wilaya.

"Mashauri ya nidhamu yamepungua sana kwa katika Wilaya yetu. Kwa miaka ya hivi karibuni hatujawahi kuwa na mashauri zaidi ya matatu kwa mwaka, hata ukiangalia kwa mwaka huu wa fedha ambao hatuna shauri hata moja kwa upande wa Wilaya na hata kwenye shule zetu," Alisema Bahebe.

Aliongeza kuwa mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na juhudi zinazofanywa na ofisi yake katika kutoa elimu kwa walimu kuhusu umuhimu wa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayosimamia kada ya ualimu.

Alifafanua kuwa yeye pamoja na watumishi wenzake katika ofisi hiyo wamekuwa na utaratibu wa kufanya ziara rasmi na zisizo rasmi kwenye shule wanazozisimiamia jambo ambalo limefanya walimu kuendelea kuwa makini na kuzingatia maadili ya kazi muda wote.

"Tunafanya ziara mara kwa mara, kwa mfano mimi na maafisa wenzangu tunaweza tukaamua kugawana shule zinazotuzunguka, asubuhi kila mtu anapitia shule moja kwa dakika chache kuangalia nini kinaendelea hapo. Walimu wakiona hivyo muda wote wanakuwa makini katika kuzingatia sheria. Hii imetusaidia sana kupunguza ukiukwaji wa maadili,"alisema.

Bahebe ameongeza kuwa sababu nyingine ya mafanikio hayo ni utaratibu wa kupokea taarifa za masuala ya nidhamu kila mwezi kutoka kwa wakuu wa shule kitu ambacho kinasaidia ofisi yake kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kudhibiti viashiria vya utovu wa maadili kwa haraka kabla ya kuchukua hatua za kisheria.

"Tumewaelekeza wakuu wa shule namna ya kuandaa taarifa ya masuala ya nidhamu na kuiwasilisha kwetu kila mwezi. Pale tunapoona kuna dalili za utovu wa nidhamu tunachukua hatua haraka za kuwafikia wahusika na kuwapa elimu kabla hatujachukua hatua kwa mujibu wa sheria," alisema Bahebe.

Pamoja na Mafanikio hayo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo anaeleza kuwa zipo changamoto ndogondogo za kinidhamu ikiwemo baadhi ya walimu kuvaa mavazi yasiyoendana na taratibu za utumishi wa umma na zile za utumishi wa walimu.

"Hapa ni mjini na nikaribu na Jiji la Dar Es Salaam, sasa kama unavyojua mjini kuna mwingiliano sana, wapo baadhi ya walimu wetu ambao wanachukua tabia za mtaani na unakuta wakati mwingine wanazileta shuleni. Hilo kwa kweli tumeendelea kulikemea na walimu wanatuelewa. Alisema Bahebe.



*Mtumishi wa TSC Wilaya ya Kibaha, Pediganda Mrosso akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake.*

# KATIBU TSC AWATAKA WALIMU KUTUMIA CHOMBO HICHO KUWASILISHA MALALAMIKO NA RUFAA ZA MASUALA YA UTUMISHI

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

KATIBU wa Tume ya Utumishi wa Walimu nchini (TSC) Paulina Mkwama amewataka walimu wote nchini walio katika Utumishi wa Umma kukata rufaa katika Tume hiyo pale wasiporidhika na adhabu wanazopewa kutokana na kufanya makosa mbalimbali ili rufaa hizo ziweze kushughulikiwa na siyo vinginevyo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu majukumu ya TSC kwa njia ya mtandao katibu huyo amesema kuwa mwalimu aliye katika Utumishi wa Umma anapoona hajaridhika na adhabu iliyotolewa na mamlaka yake ya nidhamu ngazi ya wilaya anapaswa kukata rufaa makao makuu ya TSC ambapo akiona bado hajaridhika anapaswa kukata rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Amesema kumekuwa na changamoto kwa baadhi ya walimu wanapoadhibiwa na mamlaka zao za nidhamu ,badala ya kukata rufaa na kwa kufuata taratibu zilizopo ,wanaenda kutoa malalamiko yao kwa vyombo ambavyo havihusiki nao.

"Kama mwalimu ameadhibiwa na mamlaka yake ya nidhamu ngazi ya wilaya anapaswa kukata rufaa Makao Makuu ya TSC ,lakini pia akiona bado hajaridhika na uamuzi uliotolewa na Makao Makuu anayo haki ya kuakata rufaa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na siyo kwenda kulalamika mahali popote anapoamua yeye."amesema Mkwama

Aidha amesema,moja ya jukumu la TSC ni kuwasimamia walimu walio katika utumishi wa umma katika masuala mbalimbali yakiwemo ya kinidhamu huku akibainisha baadhi ya makosa ambayo yanaweza kumtia mwalimu hatiani kuwa ni pamoja na mwalimu kukataa uhamisho,mwalimu kutoripoti kazini,mwalimu kufanya vitendo vya ukatili kwa watoto,mwalimu kung'ang'ania kituo cha awali , mwalimu kushindwa kutekeleza majukumu aliyopewa na mwajiri wake pamona na uzembe kazini .

Mkwama amesema,kwa mwalimu anayebainika kufanya makossa mbalimbali anaweza kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo,kushushwa cheo,kushushwa mshahara ama kufukuzwa kazi.

Kiongozi huyo amezungumzia kuhusu maadili ya mwalimu huku akisema,mwalimu anapaswa kuwa katika haiba nzuri inayoendana na maadili ya ualimu katika mavazi na muonekano wake wa ujumla.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwa katika mkutano na waandishi wa Habari kwa njia ya Mtandao, upande wa kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami na upande kulia ni Afisa Habari, Adili Mhina.*

# TSC YAJIVUNIA KUIMARIKA KWA HALI YA NIDHAMU ZA WALIMU BAGAMOYO NA CHALINZE



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Shauri Selelenda (kulia) akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Gerard Chami wakati Mkuu huyo wa Kitengo alipotembelea Ofisi ya Mkurugenzi huyo hivi karibuni.*

**Na. Mwandishi Wetu, Bagamoyo**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Bagamoyo inajivunia kuimarika kwa nidhamu za walimu katika halmashauri ya Bagamoyo na Chalinze ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa bidii na kufuatilia miongozo yote ya kufundishia na kujifunzia kama kuandaa maazimio ya kazi, maandalio ya somo na nukuu za somo.

Akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, hivi karibuni akiwa ziarani katika mikoa ya Pwani, Tanga, na Kilimanjaro, Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Bagamoyo, Ndg. Titus Ndomba, alisema; ofisi yake inajivunia katika usimamizi madhubuti na utoaji elimu ya maadili ya ualimu kwa walimu jambo lililopelekea kuimarika kwa hali ya nidhamu na kushusha idadi ya mashauri wanayopokea kutoka zaidi ya 100 mwaka 2017/18 hadi mashauri yasiyozidi 60 mwaka 2020/21.

KKM Ndomba alisema; "Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu 2021/22 ofisi yangu imepokea jumla ya mashauri ya kinidhamu ya walimu 18 yanayohusiana na utoro kazini, vyeti bandia, lugha chafu, na kuchangisha fedha za mafunzo ya ziada kwa wanafunzi (Tuition), ambapo mashauri yote 18 yameshatolewa uamuzi na Kamati ya Wilaya kwa walimu husika kupewa onyo, kupunguziwa mshahara na wengine kufukuzwa kazi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma kwa ujumla wake kutokana na utoro wa kudumu kazini."

Pamoja na hilo KKM Ndomba alisema katika kuongeza jitihada zaidi za kupunguza mashauri ya kinidhamu na maadili, ofisi yake iliwajengea uwezo walimu wa ajira mpya za Desemba, 2020 na Julai, 2021 kwa kuwaelimisha



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Gerard Chami (kushoto) akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo pamoja Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Bayamoyo, Titus Ndomba hivi karibuni.*

# TSC YAJIVUNIA KUIMARIKA KWA HALI YA NIDHAMU ZA WALIMU BAGAMOYO NA CHALINZE

juu ya maadili ya ualimu na nidhamu kazini kabla ya kwenda katika vituo vyao vya kazi jambo lililoleta mtazamo na matokeo chanya katika kupunguza mashauri ya kinidhamu katika eneo la Bagamoyo na Chalinze yanayohudumiwa na Ofisi ya TSC Bagamoyo.

Vilevile KKM Ndomba alisema Ofisi ya TSC Bagamoyo inahudumia jumla ya walimu 2,730 (Bagamoyo ikiwa na jumla ya walimu 1,210; Msingi walimu 698 na Sekondari walimu 512 huku Chalinze ikiwa na jumla ya walimu 1,520; Msingi walimu 942 na Sekondari walimu 578), idadi aliyosema inajumuisha walimu 73 wa ajira mpya kwa mgawanyo wa Bagamoyo walimu wanne (Msingi mwalimu mmoja na Sekondari walimu watatu) huku Chalinze ikipata walimu 69 (Msingi walimu 33 na Sekondari walimu 36) ambao wote kwa ujumla wao tayari wamepewa barua za ajira na kuanza kupokea mshahara.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo amesema Idara ya Elimu Msingi na Sekondari katika Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo na Chalinze zimekua na ushirikiano wa kuridhisha katika kushughulikia masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya kisekta ikiwa ni pamoja na kutoa nafasi kwa TSC kuwasilisha mada za kujengeana uwezo na kukumbushana mambo mbalimbali yanayohusu majukumu ya Kisheria ya TSC ambayo ni; Ajira, Nidhamu, na Maadili katika Utumishi wa Walimu nchini.

Aidha, KKM Ndomba alikishukuru Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya kwa ushirikiano mkubwa na mtazamo chanya kwa Tume katika kushughulikia masuala mbalimbali ya walimu wilayani Bagamoyo na Chalinze jambo linalopunguza ulimbikizaji na kuongezeka kwa madai na malalamiko mbalimbali ya walimu katika eneo la Bagamoyo na Chalinze.

Ofisi ya TSC Bagamoyo inahudumia halmashauri mbili za Bagamoyo na Chalinze zikiwa na jumla ya shule 176; Bagamoyo shule 46 ikiwa ni 36 za Msingi na 10 za Sekondari huku Chalinze ikiwa na shule 128 ambazo 108 niza Msingi na 20 za Sekondari.



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Bagamoyo wakiwa ofisini kwao.*

# TSC KUSARAWE WASHUKURU KWA KUWEZESHWA VITENDEA KAZI, MAFUTA NA UKARABATI WA JENGO LA OFISI



*Mkuu wa Kitengio cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami (kulia) akiongea na Afisa wa TSC Wilaya ya Kisarawe, Sophia Kizenga kuhusu maendeleo ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.*

**Na. Mwandishi Wetu, Kisarawe**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kisarawe imeishukuru TSC Makao Makuu kwa kuwezeshwa kutoa huduma bora kwa walimu baada ya kuboreshewa mazingira ya kufanyia kazi.

Shukrani hizo zimetolewa hivi karibuni na afisa wa TSC Wilaya ya Kisarawe, Sophia Kizenga kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi wa Wilaya hiyo wakati Jarida la Sauti ya TSC lilipotembelea ofisi hiyo kwa lengo la kujua maendeleo yaliyofikiwa katika kutoa huduma kwa walimu.


Kizenga alianza kwa kueleza kuwa TSC Kisarawe ina shule za msingi 86 na shule za sekondari 19 za serikali ambazo zina jumla ya walimu 814 wa shule za msingi na 628 wa sekondari ambao wanahudumiwa na ofisi hiyo kwa mujibu wa sheria.

Alisema kuwa kwa kipindi cha nyuma ofisi waliyokuwa wanaitumia ilikuwa imechakaa sana kiasi cha kutishia usalama wao pamoja na nyaraka mbalimbali za walimu.



*Mwonekano wa jengo la ofisi za TSC Wilaya ya Kisarawe baada ya kufanyiwa ukarabati na TSC Makao Makuu.*

# TSC KUSARAWE WASHUKURU KWA KUWEZESHWA VITENDEA KAZI, MAFUTA NA UKARABATI WA JENGO LA OFISI



*Mmoja wa watumishi wa TSC Kisarawe akiwa anaendelea kutekeleza majukumu ofisini kwakwe.*

"Jengo letu lilikuwa halifai kwa kweli, tulikuwa tunakaa kwa mashaka sana hata usalama wa nyaraka za walimu haukuwa mzuri. Tunashukuru sana kwa kuwa TSC Makao makuu waliliona hilo na kuamua kufanya ukarabati, hadi sana unaona ofisi ni nzuri, ina hadhi na inavutia kufanya kazi," alisema.

Aliongeza kuwa pamoja na ukarabati huo, TSC Makao makuu imepeleka vitendea kazi vya kisasa ikiwemo meza, printer, kopyuta, Viti, kabati za kutunzia nyaraka na shajala kitu ambacho kimesababisha ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa Afisa huyo upatikanaji wa vitendea kazi hivyo umesababisha mazoezi ya upandishaji madaraja, kubadilishia kazi walimu waliojiendeleza, kushughulikia ajira mpya za walimu pamoja na kuthibitisha kazini walimu yafanyike kwa haraka na kwa wakati.

"Ukiangalia mwezi Juni, 2021 tulipandisha madaraja walimu 447 wa shule za msingi na 274 wa shule za sekondari, tumeajiri walimu 40 mwezi Julai 2021 na siku chache zilizopita Kamati ya Wilaya imekaa na kuwathibitisha kazini walimu 28 walioajiriwa mwezi Desemba 2020. Fikiria hawa wote lazima wapate barua zao na mchakato wa kuwapatia hizo barua unategemea uwepo wa vifaa vya kutosha, na kwa kuwa tulikuwa navyo, hatukukwama hata kidogo," alisema Kizenga.

Aliendelea kueleza kuwa ofisi yake imekuwa ikipokea mafuta ya magari kutoka TSC Makao Makuu, kitu ambacho kimesaidia watumishi hao kufanya ziara kwenye shule mbalimbali na kukutana na walimu kwa lengo la kutoa elimu juu ya sheria na taratibu zinazosimamia utumishi wa walimu.

Alifafanua kuwa pamoja na kwamba ofisi hiyo haina magari, mafuta hayo wanayatumia kwenye magari ya Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kisarawe kwa ajili ya kufanya ziara kwenye shule mbalimbali kitu ambacho kimesaidia kuimarisha nidhamu kwa walimu.

"Unajua tukiomba gari kwa Mkurugenzi anatupatia lakini mafuta ni lazima tuweke wenyewe. Zamani tulikuwa tunashindwa kuwafikia walimu kulingana na jiografia ya Wilaya hii, lakini kwa sasa tunatembelea kata mbili kwa siku na kukutana na walimu," alisema afisa huyo.

Aliongeza kuwa, "kutokana na ziara hizo hali ya nidhamu kwa walimu inaendelea kuimarika na mashauri ya nidhamu yanazidi kupungua kia mwaka. Ukiangalia mwaka 2017/2018 tulikuwa na mashauri 39 lakini hadi kufikia mwaka 2020/2021 yalikuwa yamepungua hadi kufikia mashauri 5."

Vilevile, Kizenga amesema kuwa kutokana na kuwepo wa vitendea kazi, ofisi yake imefanikiwa kuandaa kabrasha la maadili na miiko ya kazi ya ualimu na kusambaza katika shule zote za wilaya hiyo ili kuendelea kuwakumbusha walimu kile wanachotakiwa kuzingatia kwa mujibu wa taratibu.

Afisa huyo alihitimisha kwa kueleza kuwa kwa sasa walimu wa Wilaya ya Kisarawe wanaifahamu vizuri TSC na majukumu yake na pia wanatambua na kuridhishwa na huduma zinazotolewa na ofisi hiyo.

# KATIBU TSC ATOA SIKU SABA KWA SEKRETARIETI YA KAMATI MPYA YA UKAGUZI WA NDANI YA TUME KUWASILISHA KWAKE TAARIFA YA KILA KIKAO CHA KAMATI HIYO

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa hotuba ya uzinduzi wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC uliofanyika katika Ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama, ndc, ameitaka Sekretarieti ya Kamati Mpya ya Ukaguzi wa Ndani ya Tume kuwasilisha kwake taarifa/ muhtasari wa kila kikao cha Kamati kinachofanyika ndani ya siku saba mara baada ya kikao kufanyika ili kurahisisha usimamizi madhubuti wa maazimio, maelekezo na yatokanayo ya vikao husika.

Mwalimu Nkwama aliyasema hayo hivi karibuni alipoalikwa kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa Kamati Mpya ya Ukaguzi wa Ndani ya Tume ya Utumishi wa Walimu katika Ofisi za Tume Makao Makuu, jijini Dodoma.

"Taarifa na Mihtasari ya vikao mbalimbali na hasa Kamati hii ya Ukaguzi wa Ndani ni muhimu sana katika kusimamia utekelezaji wa maazimio, maelekezo, na miongozo inayotolewa na wataalamu katika eneo hili. Naelekeza na kuisisitiza



*Mwenyekiti mpya wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC, Ally Rashid akitoa neno la Kumkaribusha Katibu wa TSC ili azindue Kamati hiyo. Hafla ya uzinduzi huo ilifanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC, Ally Rashid (kulia) pamoja na Katibu wa Kamati hiyo Laurence Chankan.*

# KATIBU TSC ATOA SIKU SABA KWA SEKRETARIETI YA KAMATI MPYA YA UKAGUZI WA NDANI YA TUME KUWASILISHA KWAKE TAARIFA YA KILA KIKAO CHA KAMATI HIYO

Sekretarieti ya Kamati hii mpya kuwasilisha kwangu muhtasari wa kila kikao cha Kamati hii ili kuweza kusimamia vema na kwenda na wakati katika utekelezaji wa yale yote yatakayokua yameazimiwa, yameelekezwa au kushauriwa na Kamati." Alisema Katibu Mw. Nkwama

Akiongezea Katibu huyo wa TSC alisema kuwa lengo la utekelezaji wa kuundwa kwa kamati hiyo ya ukaguzi wa ndani wa hesabu katika taasisi za umma ni kuzuia kwa wakati na kudhibiti mianya na dalili zozote za ubadhirifu unaoweza kubainika mapema katika matumizi ya fedha za umma ndani ya Tume na ndiyo maana Kamati hizo ni muhimu sana katika utendaji wa taasisi.

Mwl. Nkwama alisema uwepo wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani inayojumuisha wajumbe kutoka nje ya Tume utasaidia na kuongeza nafasi na umakini katika kupata hati safi kila mwaka na kuepukana na hati zenye mashaka au chafu kutokana na kutofuata taratibu mbalimbali za matumizi sahihi ya fedha za Umma ikiwa ni pamoja na kutofuata miongozo mbalimbali ya matumizi ya fedha za Umma iliyopo.

Katibu huyo wa TSC alisema mafanikio ya TSC katika utendaji wake wa majukumu ya kila siku unaitegemea sana Kamati hiyo na hivyo kuahidi ushirikiano wa kutosha usiku na mchana ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufasaha unaotakiwa.

Aidha, Mwl. Nkwama aliwapongeza Mwenyekiti, katibu na Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kuteuliwa akisema kuwa zoezi la uteuzi halikua rahisi kutokana na wote waliopendekezwa kuwa na uwezo, vigezo, na sifa za kuweza kuteuliwa na kuwemo katika kamati hiyo.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC, Ally Rashid (wa tatu kutoka upande wa kulia), Katibu wa Kamati hiyo Laurence Chankan (wa pili kutoa kushoto) pamoja na wajumbe wa Kamati hiyo.*

Kabla ya kuzindua rasmi Kamati hiyo, alitumia fursa ya uzinduzi huo kumpongeza na kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuendeleza uhamasishaji wa mapambano dhidi ya janga la UVIKO-19 baada ya kuongoza zoezi la chanjo miezi kadhaa iliyopita huku akiisisitiza Kamati kufuata maelekezo yote yanayotolewa na wataalamu wa Afya pamoja na maelekezo ya Viongozi wa Juu wa Serikali ikiwa ni pamoja na kuwasihi wananchi kupata taarifa kutoka vyanzo rasmi vya Serikali.

Nae Mwenyekiti Mpya Mteule wa Kamati hiyo mpya ya Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali ndani ya TSC, Ndg. Ally Rashid, kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama, ndc, aliyaelezea kwa ufupi majukumu ya Kamati hiyo kwa mujibu wa Sheria inayoelekeza kuundwa kwa Kamati hizo ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa wajumbe wa kamati hiyo na Menejimenti ya TSC kwani kuna nyakati zitahitaji ushiriki wa mjumbe au wajumbe wa Menejimenti kulingana na hoja itakayokuwa mezani.

# KATIBU TSC ATOA SIKU SABA KWA SEKRETARIETI YA KAMATI MPYA YA UKAGUZI WA NDANI YA TUME KUWASILISHA KWAKE TAARIFA YA KILA KIKAO CHA KAMATI HIYO



*Wajumbe pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya TSC wakiwa kwenye kikao cha uzinduzi wa Kamati hiyo kilichofanyika hivi karibuni katika Ukumbi wa TSC Makao Makuu Dodoma hivi karibuni.*









*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akikabidhi nyaraka zinazoongoza Kamati ya Ukaguzi wa Ndani kwa Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi wa Ndani mara baada ya kuzindua Kamati hiyo hivi karibuni.*

# TSC YAFANYA KIKAO NA WADAU WA ELIMU

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya kikao na wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo la kuangalia namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu.

Mkutano huo ulifanyika hvi karibuni jijini Dodoma na ulihudhuriwa na wajumbe mbalimbali wakiwemo kutoka Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Katika kikao hicho masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wa walimu yalijadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi ili kuhakikisha mwalimu hapati usumbufu katika kufuatilia masuala yake ili aongeze nguvu zaidi katika kufundisha wanafunzi.







*Wajumbe wa kikao cha wadau wa elimu wakiwa wanaendelea na kikao.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (aliyekaa mbele) akiongoza kikao cha wadau wa Elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape akitoa mchango wa mawazo wakati wa kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma, pembeni yake (upande wake wa kulia) ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*

# KIKAO CHA WAKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Menejimenti ya Tume na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kikichofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa TSC.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Menejimenti ya Tume na Wakaguzi wa Nje kikichofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa mikutano wa TSC. Upande wa kushoto ni baadhi ya wakaguzi kutoka Ofisi ya mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanaoendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za TSC.*



*Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakiwa kwenye kikao na Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (hawapo pichani) kilichofanyika hivi karibuni jijini Dodoma.*

# MSABAHA: WAAJIRI WASIFUNGE MISHAHARA YA WALIMU BILA KUZINGATIA SHERIA

**Na. Mwandishi Wetu, Korogwe**

Waajiri wameshauriwa kuzingatia taratibu zilizopo kwa mujibu wa sheria kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu ikiwemo kuwatoa walimu kwenye orodha ya mishahara kabla ya kuwasiliana na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambayo ndiyo yenye mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa walimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe, Angelina Msabaha wakati akizungumza na Jarida la Sauti ya TSC ofisini kwake mjini Korogwe.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe, Angelina Msabaha (kulia) akisisitiza jambo wakati wa mazungumzo yake na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami hivi karibuni.*

Msabaha alisema kuwa pale mwajiri anapobaini kuwa mwalimu amekosea sheria inamtaka kuwasilisha suala husika kwenye mamlaka ya nidhamu ili hatua zichukuliwe na hatimaye kufikia uamuzi wa shauri husika kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu za Utumishi wa Walimu.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe, Angelina Msabaha akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa ziara ya kiongozi huyo aliyoifanya katika ofisi za TSC Korogwe hivi karibuni.*

"Tunaendelea kuwahimiza watendaji kutoka ofisi ya mwajiri kuwa wasichukue hatua za kumuondoa mwalimu kwenye orodha ya mshahara bila kuwasilisha suala husika kwetu. Haipendezi kukuta mwalimu ameondolewa kwenye orodha ya mshahara wakati hata hajafunguliwa shauri, na pale anapofunguliwa shauri unakuta mwalimu hana hatia, hapa inakuwa tumemwonea mwalimu," alisema Msabaha.

Pamoja na hayo, Msabaha ameshauri kuwa ni vyema viongozi wanaosimamia elimu hususan maafisa elimu kuwa washauri wa walimu na pale wanapoona mwalimu anakwenda kinyume na maadili ya kazi yake wamwite na kumwelimisha kabla

# MSABAHA: WAAJIRI WASIFUNGE MISHAHARA YA WALIMU BILA KUZINGATIA SHERIA

kabla ya kuamua kuchukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria.

"Nimekuwa nikisisitiza pia kuwa maafisa elimu wana nafasi kubwa ya kuwasaidia walimu wasiingie kwenye matatizo ya utovu wa nidhamu. Ni vizuri pale anapoletewa taarifa na Mkuu wa Shule kuwa mwalimu amekwenda kinyume na taratibu, amtafute mwalimu huyo na kumshauri badala ya kushauri tu mwalimu achukuliwe hatua za kinidhamu, tusipoweka jitihada za kuwaelimisha tutajikuta tunafukuza walimu wengi," alisema Msabaha.

TSC Korogwe inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji Korogwe na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na inahudumia jumla ya walimu 817 ambao wanafundisha shule 38 katika Halmashauri ya Mji na walimu 1580 wanaofundisha shule 166 katika Halmashauri ya Wilaya.

Akizungumzia suala la uhusino kati ya Ofisi yake na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili, Msabaha alisema kuwa kuna ushirikiano mzuri kitu ambacho kimesababisha kazi nyingi kufanyika kwa wakati na kwa ufanisi.

"Tuna ushirikiano mzuri, hata ukiangalia kwenye zoezi la kupandisha madaraja walimu tulifanya kazi kwa pamoja na tulipandisha walimu 395 wa Korogwe Mji na walimu 607 wa Halmashauri ya Wilaya. Hata kwenye miradi ya ujenzi wa madarasa inayoendelea sasa, tunapata fursa ya kufanya ziara na kuongea na walimu wetu ambao ndio wanaosimamia miradi hiyo, tunawasisitiza kuzingatia maadili ya kazi na uzalendo ili miradi ikamilike kama ilivyopangwa," alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Wilaya ya Korogwe ipo katika Mkoa wa Tanga na inapakana na Wilaya za Muheza (upande wa mashariki), Wilaya ya Same (magharibi), Wilaya ya Wilaya ya Lushoto (Kaskazini) na Wilaya na Muheza (kusini) na ina ukubwa wa kilomita za mraba 3756.



*Mmoja wa Maafis wa TSC Korogwe, Joseph Shelukindo akiwa ofisini kwake.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwaongoza kikosi kazi cha kuhakiki taarifa za Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali Nchi nzima baada ya taarifa hizo kuwasilishwa na ofisi za TSC ngazi ya Wilaya.*



*Kikosi kazi maalaum cha kuhakiki taarifa za Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali Nchi nzima kikiwa kinaendela na kazi baada ya taarifa hizo kuwasilishwa na ofisi za TSC ngazi ya Wilaya.*



*Kikosi kazi maalaum cha kuhakiki taarifa za Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali Nchi nzima kikiwa kinaendela na kazi baada ya taarifa hizo kuwasilishwa na ofisi za TSC ngazi ya Wilaya.*

# TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WILAYA YA KIGOMA YAZIPONGEZA SHULE ZA SERIKALI ZILIZOONGOZA KATIKA MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA WA DARASA LA SABA MWAKA 2021

**Na. Mwandishi Wetu, Kigoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kigoma imetoa vyeti vya pongezi kwa shule mbili za Msingi za Serikali zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya Mtihani wa Taifa wa darasa la saba mwaka 2021 ikiwa ni nisehemu ya kutekeleza maelekezo ya Menejimenti ya TSC Makao Makuu iliyoelekeza ofisi za Wilaya kujenga utamaduni wa kuwapongeza walimu wanaofanya vizuri.

Shule hizo zilizopewa vyeti vya pongezi Kisozi iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliyotembelewa tarehe 18.11.2021 na Shule ya Msingi Burega iliyoko katika Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji iliyotembelewa tarehe 19.11.2021.

Katika taarifa yake aliyoituma kwa njia ya mtandao, Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC wilaya ya Kigoma, Obadia Makoko alieleza kuwa ofisi yake iliona umuhimu wa kutoa vyeti vya pongezi kutokana na juhudi zinazofanywa na walimu wa shule hizo licha ya kuwa wapo wachache.

"Shule ya Msingi Kisozi ilianza mwaka 1997, ni miongoni mwa shule 106 za Msingi za Serikali za Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma. Shule hii inatakiwa kuwa na walimu 11 lakini ina walimu watano (5) na wanafunzi 504, hivyo ina upungufu ya walimu 6, lakini pamoja na changamoto hiyo ya upungufu wa walimu shule hii imefaulisha wanafunzi kwa 100% mwaka 2020 na 2021," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa hiyo iliendelea kueleza kuwa, "Shule ya Msingi Burega ilianza mwaka 2003. Ina walimu 21 na wanafunzi 1111. Kwa miaka mitatu mfululizo shule hii imeshika nafasi ya kwanza kati ya shule 45 za Serikali za Manispaa Kigoma/Ujiji."




*Mmoja wa Walimu kiwa ameshikilia cheti cha pongezi kilichotolewa na TSC Kigoma.*

Sambamba na hayo, Kaimu Katibu Msaidizi huyo aliyekuwa ameambatana na Afisa wa TSC, Mwalimu Filbert Lukondo alipata nafasi ya kuongea na wanafunzi wa darasa la sita ambapo aliwahamasisha kusoma kwa bidii, kuacha utoro na kuepuka vishawishi vinavyoweza kuwasababishia kuingia kwenye vitendo vya ngono.

Aidha, Kiongozi huyo aliwapongeza walimu wa shule hizo kutokana na juhudi zao katika kuwafundisha wanafunzi huku akiwasihi kuendelea na moyo wa kujitolea na uzalendo ili wanafunzi waendelee kufanya vizuri katika masomo yao.

# PICHA MBALIMBALI WAKATI WA KUFUNGA MAFUNZO YA WATUMISHI WA TSC WA KADA SAIDIZI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akipokea kitini kutoka kwa Mratibu wa Mafunzo ya Watumishi wa Kada Saidizi kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma. Kitini hicho kina mada mbalimbali zilizotolewa wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 8-10 Novemba, 2021 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimali Watu, Shani Kamala akitoa neno fupi wakati wa kufunga mafunzo ya Watumishi wa Kada Saidizi wa TSC yaliyofanyika tarehe 8-10 Novemba, 2021 jijini Dodoma.*



*Baadhi ya Washiriki wa Mafunzo wa Watummishi wa Kada Saidizi wa TSC wakitoa neno la shukrani kwa Katibu wa TSC (hayupo pichani) wakati wa kufunga mafunzo hayo.*



*Baadhi ya Watumishi wa TSC wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa kufunga mafunzo.*

# PICHA MBALIMBALI WAKATI WA KUFUNGA MAFUNZO YA WATUMISHI WA TSC WA KADA SAIDIZI









*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto) akikabidhi vyeti kwa watumishi wa kada saidizi wakati wa TSC wakati wa kufunga mafunzo hayo yaliyofanyia tarehe 8-10 Novemba, 2021 jijini Dodoma.*

# TSC SAME NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

**Na. Mwandishi Wetu, Same**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Same inahudumia jumla ya Shule 230 ambapo Shule za Msingi ni 187 na Sekondari ni 43 huku shule hizo zikiwa na walimu wapatao 2079, na katika idadi hiyo walimu 1284 ni wa msingi na 795 ni wa sekondari.

Godfrey Sebulu ni Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Same, anaeleza kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 ofisi yake ilipokea na kuajiri walimu 58 na mwaka 2021/2022 ilipokea na kuajiri walimu 192 kati ya 198 waliopangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Sebulu anafafanua kuwa walimu wote walioajiriwa walipewa mafunzo elekezi juu ya Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu, haki na wajibu wao pamoja na miiko na maadili ya kazi ya ualimu kabla ya kujaza fomu za ajira na mikataba ya kazi.

Kwa upande wa upandishji madaraja walimu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ofisi hiyo ilipandisha madaraja walimu 903 ambapo walimu wa Shule za Msingi walikuwa 356 na Sekondari walikuwa 547 huku walimu 101 wakibadilishiwa kazi baada ya kujiendeleza kielimu.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Gerard Chami (kushoto) akiongea na watumishi wa TSC Wilaya ya Same wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

Katika kuangalia suala la uwiano wa walimu katika shule za msingi na sekondari zinazohudumiwa na TSC wilayani hapo, Sebulu anaeleza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Same inakabiliwa na upungufu wa walimu 928 ambapo katika idadi hiyo walimu 739 ni wa shule za msingi na 189 ni wa shule za sekondari huku upungufu mkubwa ukiwa ni kwa walimu wa masomo ya sayansi.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Same, Godfrey Sebulu (aliyesimama) akimwonesha jambo Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Gerard Chami wakati kiongozi huyo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni kwa lengo la kutaka kujua utekelezaji wa majukumu ya Tume wilani hapo.*

Katika suala la mashauri ya nidhamu kwa walimu, ofisi hiyo ilianzisha mashauri 7 ambapo mashauri 5 kati ya hayo yalihusu utoro kazini na mashauri mawili yalihusu kughushi vyeti, hata hivyo Kaimu Katibu huyo aliongeza kuwa juhudi za kutoa elimu kwa walimu zinaendelea ili kuhakikisha nidhamu ya walimu inaendelea kuimarika.

Sebulu anaendelea kueleza kuwa changamoto anayoiona katika utendaji kazi wa ofisi yake ni baadhi ya wakuu wa shule kutozingatia maadili ya uongozi katika utumishi wa umma hasa katika kusimamia maadili, nidhamu na mahusiano kazini kwa walimu wanaowasimiamia kitu ambacho kinasababisha migogoro kazini inayoathiri ufundishaji wa wanafunzi.

Kiongozi huyo anahitimisha mazungumzo yake na jarida hili kwa kueleza kuwa Tume hiyo imeendelea kupata ushirikiano kutoka katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kitu ambacho kimefanya walimu kuendelea kuhudumiwa na kutatuliwa changamoto zao kwa wakati.

# WAAJIRI WAJIBU BARUA ZA WALIMU KWA WAKATI: KAIMU KATIBU MSAIDIZI TSC ROMBO

**Na. Mwandishi Wetu, Rombo**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo Emmanuel Mwaimu amesema kuwa moja ya njia za kumsaidia mwalimu kutoingia kwenye makosa ya kinidhamu ni ofisi ya mwajiri kuji barua za walimu kwa wakati.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Rombo, Emmanuel Mwaimu akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Masiliano ya Serikali, Gerard Chami (hayupo pichani) akiwa ofisini kwake Wilayani Rombo.*

Alisema kuwa walimu wana maombi mbalimbali wanayoyawasilisha kwa mwajiri ili kupata kibali ikiwa ni utaratibu wa kawaida katika utumishi wa umma ambapo mwajiri naye ana wajibu wa kutekeleza wajibu wa kumjibu mtumishi wake.

Mwaimu anaeleza kuwa wakati mwingine walimu wanaweza kujikuta wameingia katika makosa ya kinidhamu kutokana na kuchukua uamuzi wa kufanya jambo baada ya kusubiri majibu ya maombi yao kwa muda mrefu bila mafanikio.

"Mwalimu anaweza akaandika barua ya kuomba kwenda kusoma na kuiwasilisha kwa mwajiri kwa mapema. Mwalimu huyo anaweza kusubiri ruhusa hadi muda wa kuanza masomo unafika hapati majibu, mwisho anaamua kwenda masomoni. Kisha tunaanza kumchukulia hatua kwa kosa la utoro, lakini ukiangalia kosa hilo amesababishiwa," alisema Mwaimu.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Rombo, Emmanuel Mwaimu (kulia) akiwa katika mahojiano na Mkuu wa Kitengo cha Masiliano ya Serikali, Gerard Chami hivi karibuni katika ofisi za TSC wilani Rombo.*

Mwaimu ameyaeleza hayo wakati akizungumza na Jarida la Sauti ya TSC hivi karibuni akiwa ofisini kwake wilayani Rombo wakati jarida hili lilipotembelea Wilaya hiyo kwa lengo la kujua maendeleo yaliyofikiwa katika kuwahudumia walimu.

Mwaimu ameeleza kuwa ofisi yake inapata ushirikiano mkubwa kutoka katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo kitu ambacho kimesaidia masuala mbalimbali ya walimu kufanyika kwa kuzingatia sheria kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wa walimu.

"Kwa hapa napata ushirikiano mkubwa, hata pale wanapotaka kushughulikia suala la mwalimu mara zote wananiita tushauriane namna ya kufanya. Pia TSC

# WAAJIRI WAJIBU BARUA ZA WALIMU KWA WAKATI: KAIMU KATIBU MSAIDIZI TSC ROMBO

tunaingia kwenye vikao vya Menejimeti vya Halmashauri, hivyo tunajivunia sana kwa hilo kwa kuwa limefanya tuendelee kuwahudumia walimu kwa weledi zaidi," alisema Mwaimu.

Mwaimu ameeleza kuwa Wilaya hiyo ina jumla ya Shule za Serikali 193 ambapo shule 152 ni za Msingi na Shule 41 ni za Sekondari huku shule hizo zikiwa na jumla ya walimu1889 ambapo walimu 1121 ni wa msingi na 768 ni wa sekondari.

Ameelieza kuwa kutokana ushirikiano huo kumekuwa na utulivu mkubwa wa walimu katika Wilaya hiyo kutokana na ofisi yake kukutana na walimu mara kwa mara na kuwaelimisha pamoja na kushughulikia malalamiko yao na changamoto mbalimbali za kiutumishi.

"kutokana na elimu hiyo, manung'uniko mengi ya walimu yamekuwisha. Mara nyingi walimu walikuwa na malalamiko kwa kutokujua jinsi taratibu za utumishi zinavyokwenda. Tumewaelimisha na sasa wanajua wajibu pamoja na haki zao, hivyo hata pale wanapotafuta haki zao wanazingatia taratibu zilizopo," alisema Kaimu Katibu Msaidiazi huyo.

Hata hivyo, Mwaimu alieleza kuwa, ushirikiano zaidi unahitajika kati ya TSC na Idara ya Elimu kwani wao ndio wanaohusika moja kwa moja katika kuhakikisha walimu wanapata haki zao lakini pia wanakuwa na uelewa wa kutosha juu ya maadili ya kazi yao kwa mujibu wa sheria.

masomo ya sayansi.

Katika suala la mashauri ya nidhamu kwa walimu, ofisi hiyo ilianzisha mashauri 7 ambapo mashauri 5 kati ya hayo yalihusu utoro kazini na mashauri mawili yalihusu kughushi vyeti, hata hivyo Kaimu Katibu huyo aliongeza kuwa juhudi za kutoa elimu kwa walimu zinaendelea ili kuhakikisha nidhamu ya walimu inaendelea kuimarika.

Sebulu anaendelea kueleza kuwa changamoto anayoiona katika utendaji kazi wa ofisi yake ni baadhi ya wakuu wa shule kutozingatia maadili ya uongozi katika utumishi wa umma hasa katika kusimamia maadili, nidhamu na mahusiano kazini kwa walimu wanaowasimiamia kitu ambacho kinasababisha migogoro kazini inayoathiri ufundishaji wa wanafunzi.

Kiongozi huyo anahitimisha mazungumzo yake na jarida hili kwa kueleza kuwa Tume hiyo imeendelea kupata ushirikiano kutoka katika ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kitu ambacho kimefanya walimu kuendelea kuhudumiwa na kutatuliwa changamoto zao kwa wakati.



*Mkuu wa Kitengo cha Masiliano ya Serikali, Gerard Chami (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Rombo.*

# KAIMU KATIBU MSAIDIZI WA TSC - MWANGA AWASIHI BAADHI YA WALIMU WILAYANI HUMO KUJIEPUSHA NA ULEVI ILI KUTEKELEZA WAJIBU WAO



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mwanga, Catherine Kimario akiwa ofisini kwake.*

**Na. Mwandishi Wetu, Mwanga**

Pamoja na hali nzuri ya nidhamu za walimu Wilayani Mwanga, Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wilayani humo, Ndg. Catherine Kimario, amewasihi baadhi ya walimu wilayani humo ambao wanahudumiwa na ofisi yake (TSC - Mwanga) kujiepusha na ulevi unaowasababisha kushindwa kutekeleza wajibu na jukumu lao la kuingia darasani na kufundisha.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwanga, Ndg. Catherine Kimario, wakati akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, akiwa ziarani katika mikoa ya Pwani, Tanga, na Kilimanjaro.

Alisema KKM Ndg.Kimario, "Hali ya nidhamu za walimu na utii wa nguzo kuu tano za maadili ya ualimu ni mzuri sana, ila dosari inakuja kwa baadhi ya walimu ambao hata mashauri yao yanapowasilishwa huwa kwa sehemu kubwa ni kuhusiana na ulevi uliokithiri unaowasababishia kushindwa kuingia madarasani na kutoa huduma stahiki kwa wanafunzi wao huduma ambayo ni kuwafundisha kwa mujibu wa ratiba na miongozo iliyopo."

Alisema katika mambo ambayo TSC wilayani humo inaweza kujivunia na kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, ni pamoja na kufanikiwa kuwapandisha madaraja walimu wote waliostahili kupandishwa kama walivyokasimiwa na wote kuanza kupokea mishahara mipya ya madaraja hayo.

Pamoja na hilo, Ndg. Kimario aliishukuru Tume ya Utumishi

# KAIMU KATIBU MSAIDIZI WA TSC - MWANGA AWASIHI BAADHI YA WALIMU WILAYANI HUMO KUJIEPUSHA NA ULEVI ILI KUTEKELEZA WAJIBU WAO

wa Walimu Makao Makuu kwa kuiwezesha Ofisi ya TSC – Mwanga kupata vifaa bora navya kisasa katika utendaji kazi kwa ufanisi na kumthibitishia Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kuwa walimu na wateja wengine wanaohitaji huduma ya TSC – Mwanga wanaipata huduma hiyo kwa wakati kama inavyoelekezwa katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Tume.

Aidha, KKM Ndg. Kimario alisema bado kumekuna na changamoto ya makazi kwa baadhi ya walimu hasa wanawake wanaohudumu katika mazingira na jamii za wafugaji kutokana na ufinyu wa nyumba za makazi ya walimu au kutokuwepo kabisa kwa nyumba hizo kwa mgawanyo sawa wa kijinsia kati ya walimu wanaume na walimu wanawake.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alishukuru kwa ushirikiano anaoupata kutoka Idara za Utawala, Utumishi na Rasilimali Watu, Elimu Msingi na Sekondari, Udhibiti Ubora wa shule pamoja na walimu wa wilaya hiyo na kuifanya kazi ya Tume kuwa rahisi na yenye tija katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Kisheria yaani; Ajira, Nidhamu na Maadili ya Ualimu.

Ofisi ya TSC – Mwanga inahudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Mwanga ikiwa na jumla ya shule 136 zilizosajiliwa; ikiwa Shule za Msingi ni 110 na Sekondari 26 huku ikihudumia jumla ya walimu wanaoingia darasani 1,183; ambapo jumla ya walimu 657 wanafundisha Shule za Msingi na 526 wanafundisha Shule za Sekondari, idadi inayojumuisha walimu 184 wa ajira mpya za mwaka 2019 (25), 2020 (37), na 2021 (122) ambao wote kwa ujumla wao walishapewa barua za ajira na kuanza kupokea mshahara kwa nafasi walizoajiriwa.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mwanga, Catherine Kimario (kushoto) akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami ofisini kwake hivi karibuni.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa nne kutoka kushoto) akiwa pamoja na Waziri wa Sanaa Utamaduni na Michezo, Innocent Bashungwa (wa sita kutoka kushoto) pamoja na viongozi wengine (Makatibu Wakuu, Mkuu wa Mkoa wa Mrorgoro, pamoja na Viongozi wa Shimiwi) wakiangalia mcheo wa fainali wakati wa kufunga mashindano ya SHIMIWI Novemba 2, 2021 mjini Morogoro.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka TSC, Moses Chitama akisalimia baada ya kutambulishwa wakati kwa kufunga mashindano ya SHIMIWI Novemba 2, 2021 mjini Morogoro.*




*Wanamichezo wa TSC wakiwa kwenye maandamano wakati wa kufunga mashindano ya SHIMIWI Novemba 2, 2021 mjini Morogoro.*

# KATIBU TSC AWAPONGEZA WACHEZAJI WALIOSHIRIKI MASHINDANO YA SHIMIWI



*Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiongea na wachezaji walioshiriki mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika kwa wiki mbili na kuhitimishwa Novemba, 2, 2021, mjini Morogoro.*

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama amewapongeza wachezaji wa tume hiyo walioshiriki mashindano ya SHIMWIWI yaliyofanyika kwa wiki mbili na kumalizika Novemba 2, 2021 mjini Morogoro.

Nkwama alitoa pongezi hizo wakati alipokutana na wachezaji hao hivi karibuni ambapo pamoja na mambo mengine wachezaji walimkabidhi Medali waliyoipata baada ya kuibuka mshindi wa tatu katika mbio za watumishi wenye umri wa zaidi ya miaka 55 pamoja na cheti cha kushiriki mashindano hayo.

"Ninawashukuru sana kwa



*Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akipokea cheti cha ushiriki wa mashindano ya SHIMIWI kutoka kwa Katibu wa SHIMIWI tawi la TSC, Enid Geofrey wakati Katibu huyo alipokutana na wachezaji walioshiriki mashindano hayo hivi karibuni.*

# KATIBU TSC AWAPONGEZA WACHEZAJI WALIOSHIRIKI MASHINDANO YA SHIMIWI



*Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akivishwa medali na mchezaji Bwitalihati Magota wakati Katibu alipokutana na wachezaji wa TSC walioshiriki mashindano ya SHIMIWI. Medali hiyo ilipatikana baada ya TSC kushika nafasi ya tatu katika mbio za watumishi wenye umri unaoanzia miaka 55 na kuendea.*

Katibu huyo aliwashauri wachezaji hao kuendelea kufanya mazoezi wakati wote badala ya kusubiri muda unaotolewa na ofisi kwa ajili ya kufanya mazoezi kwa kuwa licha ya kufanya mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano mbalimbali, mazoezi ni muhimu katika kuimarisha afya na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

"Ninajua mlipokuwa Morogoro mlikuwa mnafanya mazoezi kila siku asubuhi na jioni, sasa ninawaomba msiache tabia hiyo. Usifanye mazoezi pale unaposikia kuwa kuna mashindano tu, mazoezi ni muhimu katika kuimarisha afya zetu hususan sisi ambao tunatumia muda mwingi tukiwa tumekaa aofisini," alisema.

kushiriki mashindano ya SHIMIWI, ninatambua kuwa muda wa maandalizi ulikuwa ni mfupi sana lakini kila mmoja amefanya kazi yake kwa nguvu kwa lengo la kuitangaza na kuiletea heshima Tume," alisema Nkwama.

Kiongozi aliwaahidi wacezaji hao kuwa, mashindano yatakayofanyika mwakani yatakuwa na maandalizi ya kutosha kwa kuwa Tume hiyo itaandaa wachezaji mapema na kuwapatia vifaa muhimu ili waweze kurudi na makombe mengi ya ushindi.

"Ninawaahidi kuwa mwakani tutajipanga vizuri zaidi, tutafanya maandalizi mapema, tutahakikisha tunanunua vifaa vinavyohitajika na tutaendelea kuwapa muda wa kufanya mazoezi ili muweze kufanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo," alisema.



*Wachezaji walioshiriki mashindano ya SHIMIWI wakiwa katika kikao na Katibu wa TSC mara baada ya kumalizika kwa mashindano hayo yaliyofanyika mjini Morogoro.*

# TSC YAFANYA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA SHIMIWI

**Na. Mwandishi Wetu, Dodoma**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imefanya uchaguzi wa kupata viongozi wa SHIMIWI ikiwa ni mara ya kwanza tangu tume hiyo ilipoanzishwa mwaka 2016.

Uchaguzi huo uliofanyika mapema katikati ya mwezi Novemba 2021 umewaweka madarakani Gerard Chami (mwenyekiti), Mecktildis Kapinga (Makamu Mwenyekiti), Enid Geofrey (Katibu) na Pastory Mnyaki (Katibu Msaidizi).

Viongozi wengine waliochaguliwa ni Mashaka Athuman (Mhasibu) na Francis Gwankisa (Mjumbe wa Shimiwi Taifa) huku Thomas Tambilija, Sophia Kutona na Thomas Kilijumbe wakichaguliwa kuwa wajumbe wa tawi.



*Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (aliyefunika kichwa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa SHIMIWI mara baada ya uchaguzi huo kumalizika.*



*Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (aliyefunika kichwa) akiwa akitka picha ya pamoja na watumishi wa TSC walioshiriki uchaguzi wa kuwachagua viongozi wa SHIMIWI.*



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

*Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania* *tumeyautumishiwawalimutanzania*